# BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

## MKUTANO WA NANE

**Kikao cha Kumi na Sita – Tarehe 28 Septemba, 2022**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

I. TAARIFA YA SPIKA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC) kwa mwaka 2018/2019 - 2019/2020.

Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika (LAAC) kwa mwaka 2018/2019 - 2019/2020.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC):

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC) kuhusu Ripoti ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC) kwa mwaka 2018/2019 - 2019/2020.

**<u>Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika (LAAC):</u>**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika (LAAC) kuhusu Ripoti ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika (LAAC) kwa mwaka 2018/2019 - 2019/2020.

## III. <u>MASWALI:</u>

**<u>Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:</u>**

50. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Haki za binadamu ni jambo muhimu na lilipewa nafasi kubwa katika Katiba zetu zote mbili kwa maana ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 na ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Kwa kuwa Haki ya Faragha ni miongoni mwa haki za msingi za binadamu na kwa kuwa tangu 1964 hadi leo hii haki hiyo inakosekana katika Vyuo vingi vya Mafunzo hapa Zanzibar, ikiwa ni pamoja na wanafunzi zaidi ya saba kuwekwa kwenye chumba kimoja na kuwekewa ndoo kwa ajili ya kujisaidia (Mtondoo), kama ilivyo kwenye Chuo cha Mafunzo cha Wete Pemba.

Je, ni lini Serikali itatekeleza matakwa ya Katiba kwa kuwapatia haki ya faragha wanafunzi pamoja na mahabusu waliopo kwenye Vyuo mbali mbali vya Mafunzo nchini, kwa kuwajengea vyoo badala ya kuwawekea Mtondoo, ambao unatia maudhi na shida kwa wale wanaojisaidia na wale washirika wenzake waliomo chumbani.

**<u>Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:</u>**

103. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Ni jambo la kusikitisha kwamba, pamoja na kwamba Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) ni benki pekee ya Serikali hapa nchini ikiwa na malengo zaidi ya kutoa huduma kwa Serikali na watu wa Zanzibar, imekuwa ikishindanishwa na benki ambazo malengo ya kuanzishwa kwao ni tofauti na malengo ya kuanzishwa kwa PBZ. Hali hii imepelekea Benki hii kunyang'anywa shughuli za kufanya za Zanzibar kwa kisingizio cha kutokuwa na mifumo bora au uzoefu wa baadhi ya shughuli.

Je, ni kasoro zipi ilizonazo PBZ na ni upi mpango wa Serikali wa kuiboresha mifumo ya PBZ na kuipa uzoefu ili iweze kufanya shughuli ambazo kwa sasa zimepewa mabenki mengine yasiyo ya Serikali wala yasiyo ya Zanzibar.

104. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Ni jambo jema kwamba Serikali imeleta huduma ya ulipaji kodi katika Bandari ya Zanzibar kupitia kituo kimoja tu *(One Stop Centre)*. Hata hivyo, wakusanyaji na utaratibu wa ukusanyaji wa mapato hayo muhimu ya bandarini haviko wazi kwa wananchi.

Je, ni upi utaratibu wa ukusanyaji wa mapato na ugawaji wake kutoka *One Stop Centre* na ni ipi nafasi ya ZanMalipo katika uendeshaji wa *One Stop Centre.*

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

111. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kumekuwa na malalamiko kwamba meli zinazosafirisha abiria kati ya Unguja na Pemba zinakiuka sheria na taratibu za kimataifa pale abiria anapofariki akiwa ndani ya meli kama msafiri.

(a) Je, kwa miaka 10 iliyopita, ni watu wangapi wamefariki wakiwa safarini ndani ya meli kati ya Unguja na Pemba.

(b) Je, ni utaratibu upi sahihi wa kufuatwa pindi abiria anapofariki akiwa ndani ya meli inayoenda kati ya Unguja na Pemba.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

57. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Katika visiwa vya Unguja na Pemba, baadhi ya wananchi wamekuwa na utaratibu mbaya wa kukata miti ya matunda kama vile mafenesi, miembe na mishelisheli, kwa ajili ya kupasua mbao za kutengenezea samani (furnitures) mbali mbali, jambo ambalo ni hatari kwa ajili ya maisha yetu binafsi. Kwa kuwa mbao za miti kama vile Mikangazi, Mininga na Mikungu ina mbao nzima na madhubuti zaidi ukilinganisha na hizo za miti

ya matunda.

(a) Kwa nini Serikali isiwahamasishe watu kutumia zaidi mbao za mti ya Mikandazi, Mininga, Mikungu na miti mengine madhubuti zaidi kuliko ya miti yetu ya matunda.

(b) Ni lini Serikali itatoa taaluma kwa wananchi juu ya kutunza mazingira pamoja na kuihifadhi hiyo miti yetu ya matunda yenye asili ya visiwa hivi.

<u>Wizara ya Maji, Nishati na Madini:</u>

130. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Kwa kuwa maji ni uhai, na kwa kuwa mwanadamu anatakiwa kunywa maji safi na salama ili apate afya njema.

Je, ubora wa maji hasa tunayotumia kwa kunywa na kupikia unapimwaje.

148. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Ingawa changamoto ya maji safi na salama imepunguwa kwa kiasi fulani katika baadhi ya maeneo ya jimbo la Wawi.

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha kimetengwa kutatuwa changamoto ya maji kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

(b) Je, ni maeneo yepi ya jimbo la Wawi yatanufaika na fedha hizo.

<u>Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:</u>

110. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa wananchi kwamba upatikanaji wa ruzuku iliyotokana na Mradi wa ZISP, haukuwa na uhakika, bila ya wananchi hao kupatiwa maelezo ya kutosha juu ya hali hiyo.

Je, Mradi wa ZISP unaendeleaje, umefikia wapi na lini unatarajiwa kumalizika.

158. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Tunaendelea kuipongeza Serikali yetu kwa kuongeza maslahi ya walimu, ingawaje juhudi hizo bado hazijaweza kutatua changamoto ya walimu kulipwa nauli za kufika katika maeneo yao ya kazi, kwa maana ya skuli.

Je, kwa nini walimu wa msingi hawapewi nauli ya kuwafikisha kazini mwao.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

Ripoti ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC) kwa mwaka 2018/2019 - 2019/2020.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

Ripoti ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika (LAAC) kwa mwaka 2018/2019 - 2019/2020.



Zanzibar, (Raya Issa Msellem)
28 Septemba, 2022. KATIBU WA BARAZA.